# PARLIAMENT OF KENYA

## THE SENATE

## THE HANSARD

**Tuesday, 23rd July, 2019**

*The House met at the Senate Chamber,*
*Parliament Buildings, at 2.30 p.m.*

*[The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Lelegwe) in the Chair]*

PRAYER

THE DIVISION OF REVENUE BILL
(SENATE BILLS NO. 13 OF 2019)

**Sen. Pareno:** Mr. Temporary Speaker, Sir, I beg to report that the Committee of the Whole has considered The Division of Revenue Bill (Senate Bills No. 13 of 2019) and its approval thereof without amendments.

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Mover?

**Sen. (Eng.) Mahamud**: Mr. Temporary Speaker, Sir, I beg to move that House do agree with the Committee in the said report, and request Sen. Maina to second.

**Sen. (Eng.) Maina**: I second.

*(Question proposed)*

*(Question put and agreed to)*

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Mover.

**Sen. (Eng.) Mahamud:** Mr. Temporary Speaker, Sir, I beg to move that the Division of Revenue Bill (Senate Bills No. 13 of 2019) be now read a Third Time.

I ask Sen. Olekina to second.

**Sen. Olekina:** Mr. Temporary Speaker, Sir, I beg to second.

*(Question proposed)*

*(Question put and agreed to)*

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Order, Senators. I now order that the doors be closed and the bars be drawn.

*(Doors were closed and the bars drawn)*

**Sen. Olekina:** Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. I rise to support that this Message be transmitted. Today, we make history in this House as the true defenders of devolution. We want Kenyans to know that if the National Assembly delays in considering our Bill, they will be the ones denying them money. This is a House of reason---

I am quite happy to see the Clerk walking and getting ready to go and do what we have asked him to do. In fact, we should even escort him, so that we can show Kenyans that we mean business.

*(Applause)*

I would like to congratulate all my colleagues and thank you for standing up for devolution and Kenyans. When history will be written, this House and the 68 Members who make up this House, will have a big portion of the space of history in this country as having stood firm for devolution.

I support and thank you all for defending devolution.

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Order! Hon. Senators, we now proceed to Order No.7 on the Statement by Sen. Faki.

## STATEMENTS

### UJENZI WA MAKAO MAKUU YA IDARA YA UVUVI KATIKA ENEO LA SOUTH C, NAIROBI

We deferred this Statement and promised to come back to it later. There could be Senators who would wish to make their comments on it. Before I give you time to make your comments, I have two communications to make.

*(Interruption of debate on Statement)*

## COMMUNICATION FROM THE CHAIR

### VISITING DELEGATION FROM VARIOUS SCHOOLS

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Hon. Senators, I would like to acknowledge the presence in the Public Gallery this afternoon of visiting students and teachers from Kibichoi and Kiwaiguru Primary Schools in Kiambu County.

In our usual tradition of receiving and welcoming visitors to Parliament, I extend a warm welcome to them and on behalf of the Senate and on my own behalf, wish them a fruitful visit.

I thank you.

Sen. Madzayo, you may now proceed.

*(Resumption of debate on the Statement)*

**Sen. Madzayo:** Asante, Bw. Spika wa Muda. Ningependa kutoa maneno yangu kuhusiana na hii taarifa ambayo imeletwa hapa na Sen. Faki. Waswahili wanasema kwamba, ukishangaa ya Musa, nenda feri kule Likoni ndio utaona maajabu.

Bw. Spika wa Muda, ni jambo la kusikitisha katika historia ya nchi kuona Wizara nzima ambayo ina wasomi, wanaweza kufikiria kujenga makao makuu ya uvuvi, mahali kama Nairobi, South C, ilhali kuna kaunti tano za eneo la pwani ambazo ziko katika ufuo wa bahari na uvuvi wetu unaendelea huko.

**Sen. Cherargei**: Hoja la nidhamu, Bw. Spika wa Muda. Singependa kumzuia rafiki yangu, Sen. Madzayo kuzungumza, lakini kuna methali ya Kiswahili ambayo inasema "Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni." Mimi nimesikia akisema "Ukishangaa ya Musa, utaona ya feri ya Likoni". Sasa nimechanganyikiwa kidogo kwa sababu sijui kama methali hiyo umebadilishwa na wataalum wa lugha.

**Sen. Madzayo**: Asante, Bw. Spika wa Muda. Mhe. Cherargei, hawezi kuelewa misemo au methali yote ya watu wa Pwani. Kwa hivyo, mambo ya bahari ambayo kivukisho chake ni feri, pengine hicho Kiswahili kimempita na hakuelewa nilichomaanisha. Hata hivyo, ninamshukuru sana kwa kuongea Kiswahili sanifu.

Bw. Spika wa Muda, tunaona maajabu hivi sasa tunayahamisha makao makuu ya uvuvi kutoka pwani ambapo kuna bahari. Hakuna nchi yoyote katika ulimwengu ambayo imetenda kitendo kama hicho isipokuwa Kenya. Jambo la kusikitisha ni kwamba utaona watu ambao wamepewa nyadhifa kama hizo ndio wanafanya ufisadi wa hali ya juu zaidi. Ukitaka kunyanyasa watu wa Pwani, basi wewe chukua uvuvi uulete hapa Nairobi ambapo hakuna bahari wala Ziwa Victoria. Ndugu yangu Sen. Sakaja hawezi kuelewa kwa sababu anatoka Kaunti ya Nairobi Mjini. Lakini anajua ya kwamba hapa Kaunti ya Nairobi Mjini hakuna bahari wala ziwa kubwa kama Ziwa Victoria.

Bw. Spika wa Muda, tunapofikiria kujenga makao makuu ya uvuvi katika nchi hii, ni heri kufikiria maeneo ya pwani ambapo kuna bahari. Lakini utapaka kwamba mahali ambapo panatakiwa kutengenezwa huu mjengo, tayari kuna ofisi kuu ya fisheries. Kinachohitajika kuongezwa ni majengo zaidi ili watu wafaidike na shughuli za uvuvi.

Bw. Spika Wa Muda, nataka utafakari jambo hili. Wavuvi wanapata shida sana kusafiri kutoka Kaunti za Mombasa, Taita-Taveta, Kwale, Lamu na Tana River; kuja Kaunti ya Nairobi Mjini ambapo ndio makao makuu ya uvuvi. Vile vile watu wa Kaunti ya Kisumu kutoka upande za Nyanza wanalazimika kusafiri mpaka Nairobi Mjini kwa sababu ya uvuvi. Hiyo si haki. Ni haki ya watu wanaoishi katika zile kaunti tano za pwani wapewe nafasi yao ya kuwa na makao makuu ya uvuvi.

**Sen. Cherargei:** Asante, Bw. Spika Wa Muda, kwa nafasi hii. Ningependa kuunga mkono Arifa ya ndugu yangu, Seneta wa Kaunti ya Mombasa, Sen. Faki. Kama tulivyosema katika sheria ya maswala ya majani chai, kwamba makao makuu ya maswala ya majani chai yawe katika mji wa Kericho. Jambo hili linafaa kuzingatiwa pia kwa mambo ya uvuvi kwa sababu hatuoni ziwa katika Kaunti ya Nairobi Mjini. Lengo kuu la ugatuzi ni kupeleka mashinani huduma zote.

Ninamuunga mkono ndugu yangu, Sen. Faki. Ninafikiri hata sisi tunaotoka sehemu zinazopanda mahindi, tunataka pia maghala ya mahindi yawe katika mji wa Eldoret. Tukifanya hivyo, itasaidia kuleta uwiano mzuri, agenda kubwa, na azma na lengo nzuri la ugatuzi katika taifa la Kenya. Taasisi au vyombo vya Serikali au madola yanafaa kuhakikisha kwamba yamezingatia azimio ambalo Seneti inaweza kutoa

kulingana na hiyo arifa. Sisi kama kamati husika tunatarajia majibu sahihi ambayo yatasaidia kuendesha ugatuzi katika taifa letu la Kenya.

Asante, Bw. Spika wa Muda.

*(Loud consultations)*

**Sen. Sakaja**: Bw. Spika Wa Muda, wenzangu wananisihi nizumgumze Kiswahili. Hawajui ya kwamba mimi ni gwiji katika mambo ya Kiswahili sanifu na hata utohozi, ufafanuzi na falsafa za Kiswahili.

Mimi ni Seneta wa Kaunti ya Nairobi Mjini na ni kweli nimezaliwa mjini Nairobi. Wakati ambapo tulijaribu kuvua samaki, tulipata tu vyura wadogo au Tadpoles kwa Kiingereza, katika Mto Nairobi. Sen. Mutula Kilonzo Jnr. atakueleza ilikuwa hivyo katika Mto Kirichwa. Kwa kawaida, Seneta atasimama hapa kutetea jimbo lake kusema kwamba idara hii au taasisi fulani ibaki kwake. Lakini mimi kama Seneta wa Kaunti ya Nairobi Mjini, ninaienzi taifa letu, na pia ninaamini kwamba lazima tuwe na ugatuzi wa ukweli na haki.

Wale ambao walifikiria kwamba wataleta ofisi ya halmashauri ya mambo ya uvuvi mjini Nairobi, nafikiri wamepotea kabisa. Nitaomba kwamba wafikirie tena. Tuna majimbo ambayo yana uvuvi katika eneo la Pwani kama vile wenzangu walivyosema. Tuko na uvuvi katika majimbo ya eneo la Ziwa Victoria; Kisumu, Migori na Siaya. Pia uvuvi unatendeka katika Kaunti ya Turkana.

Kama kuna jambo ambalo lina umaarufu katika sehemu fulani kwa mfano, mambo ya kukuza majani chai, tuangalie majimbo ambayo yako katika maeneo ya majani chai. Kama ni mambo ya michezo kama vile mbio, tuangalie majimbo ya Nandi, West Pokot na Elgeyo-Marakwet.

Bw. Spika wa Muda, Hii taarifa iliyoombwa na ndugu yangu, Seneta wa Kaunti ya Mombasa, haifuatilizwi kwa Kamati ya Bunge la Seneti. Kwa hivyo, ningemwomba ailete kwa njia mbadala. Akifanya hivyo, kama ni jambo la Kamati ya Ukulima, Ufugaji na Uvuvi, wataweza kualika Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ukulima na waseme kwa kinaga ubaga kile wanachojaribu kufanya. Asipofanya hivyo, itakuwa ni kama tu tumezungumza na tumepaka mafuta kwa mgongo wa chupa ama tumechezea mbuzi gita.

Asante, Bw. Spika wa Muda.

**Sen. Ochillo-Ayacko**: Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir.

*(Laughter)*

I will not use Kiswahili.

Mr. Temporary Speaker, Sir, this is a very important Statement. I am speaking here in three capacities; as Senator from Lake Victoria region in Migori County where we have a beautiful lake. We have neighbouring lakes. We are fisher people by practice and behaviour. We know how to live with fish and the fish also know how to live with us.

*(Laughter)*

I want to appreciate the importance of this Statement and congratulate my brothers, Sen. Faki and Sen. Madzayo. They want resources devolved to where an

activity is. The issue being debated here is about construction of a building. I do not think that the construction of a building is what we should be fighting over. In fact, Nairobi City County should just have a coordinating office and the Ministry.

However, we want to see both operational and substantive matters in the counties that are responsible for fishing. We want to see something important going on in Mombasa, Kilifi, Kwale, Tana River, Migori, Homa Bay, Kisumu, Busia and Turkana counties. This is because it is in those counties that fishing activities are major economic and cultural activities.

Mr. Temporary Speaker, Sir, hopefully, this matter will come before the Committee on Agriculture, Livestock and Fisheries, where Sen. Madzayo and I sit. We are going to do our best to ensure that we do not bring buildings here and forget about our fishing people and their activities. Fishing in those counties is adored as a meal and an activity that generates resources. It is respected by our people.

Thank you, Sen. Faki, for raising this important social and economic matter.

*(Interruption of debate on Statement)*

## COMMUNICATION FROM THE CHAIR

### VISITING DELEGATION FROM CALVARY ACADEMY SCHOOL, KAJIADO COUNTY

**The Temporary Speaker** (Sen. (Dr.) Lelegwe): Hon. Senators, I have a Communication to make. I would like to acknowledge the presence in the Public Gallery this afternoon of visiting students and teachers of Calvary Academy School from Kajiado County.

In our usual tradition of receiving and welcoming visitors to Parliament, I extend a warm welcome to them. On behalf of the Senate and my own behalf, I welcome them and wish them a fruitful visit.

I thank you.

Proceed, Sen. Pareno.

*(Resumption of debate on Statement)*

**Sen. Pareno:** Asante, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijachangia taarifa hii, ningependa kuwakaribisha wanafunzi kutoka shule ya Calvary kutoka Kaunti ya Kajiado. Mmekaribishwa sana katika Seneti yetu; tunawaombea msome vizuri na mfaulu kimaisha. Asante kwa kuchagua kuja kujifunza katika Seneti ya Kenya.

Bw. Spika wa Muda, namshukuru ndugu yangu, Sen. Faki, kwa kuleta taarifa hii kuhusu ujenzi wa ofisi za uvuvi za kitaifa. Nmeangalia taarifa ambayo ilikuwepo katika gazeti kuhusu kandarasi hiyo na imebainika kwamba kuna wafadhili, ambao ni Benki Kuu ya Dunia, waliojitokeza na kuamua kufadhili mradi huo wa uvuvi katika Kaunti ya Kwale, Mombasa, Kilifi, Tana River na Lamu. Itakuwa maajabu iwapo Benki Kuu ya Dunia itajitokeza kufadhili kaunti tano ama kufadhili uvuvi na kuinua maisha ya wavuvi katika kaunti hizo tano, halafu Serikali ya Kitaifa iamue kwamba pesa hizo ambazo ni za

wafadhili zitumike katika kujenga ofisi Nairobi. Kufanya hivyo, itakuwa ni kudhulumu wavuvi na haifai kabisa.

Bw. Spika wa Muda, ingawa Katiba yetu imesema kwamba mambo ya uvuvi yako katika ofisi za kitaifa, basi ingefaa wale wanaopenda kujenga ofisi hizi za kitaifa hapa Nairobi watumie bajeti yao kufanya hivyo badala ya kutumia pesa za ufadhili, ambazo malengo yake yalikuwa ni kuinua wavuvi katika kaunti hizo nilizozitaja hapo awali.

Bw.Spika wa Muda, nimeelezwa kwamba tayari kuna ofisi ya utafiti katika kaunti za Pwani. Kwa hivyo, pesa hizo zingefaa kutumika kuipa nguvu ofisi hiyo ya utafiti na kazi ya uvuvi katika Pwani. Hatusemi kwamba ni wanapwani tu ndio wanaweza kufanya uvuvi; tunajua kwamba wale walio katika Ziwa la Victoria pia wanafanya uvuvi. Lakini haifai kwa msaada ambao malengo yake yalikuwa ni kaunti za Pwani urudishwe na kupelekwa katika ofisi za Nairobi.

Bw. Spika wa Muda, tunalaani jambo hilo. Ningependa Kamati itakayoshughulikia jambo hilo ihakikishe kwamba pesa hizo za wafadhili zitumike kikamilifu na kwa njia ambayo walikuwa wameamua zitatumika.

**Sen. Boy:** Asante sana, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa fursa hii. Kwanza, natoa shukrani kubwa kwa Mhe. Sen. Faki kwa kuleta taarifa hii hapa. Kusema kweli, hili ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu kama unavyojua, uvuvi nchini Kenya unafanyika sana katika upande wa Pwani, sehemu za Nyanza na Turkana.

Bw. Spika wa Muda, pia ni jambo la kusikitisha kuona kwamba makao makuu ya hizo ofisi yatajengwa hapa Nairobi. Kusema ukweli, ukiangalia wewe mwenyewe, jambo kama hili katika wakati kama huu, kama ni kweli hizo ofisi kujengwa, basi tuangalie Kilillahi na kihaki aidha zijengwe kwetu Pwani, katika sehemu za Turkana ama katika sehemu za Ziwa Victoria.

Nikiongezea, Bw. Spika wa Muda, hivi sasa kuna kiwanda kikubwa cha samaki kinachojengwa na watu kutoka China katika sehemu za Shimoni. Samaki wanavuliwa, wanawekwa kwenye *cold storage* na kusafirishwa kupelekwa nje ya nchi. Vile vile kuna miradi mingine inayoendelea sehemu za Shimoni, Mtwapa na Kilifi. I wapo wavuvi hawa kesho watakuwa na shida, watakimbilia ofisi gani? Hakuna ofisi nyingine, isipokuwa karibu ni pale sehemu za pwani.

Bw. Spika wa Muda, naunga mkono taarifa iliyoletwa na Sen. Faki. Tunataka hii Kamati itakayohusika kuchunguza shida hii waangalie kabisa. Ilifikia vipi hadi uamuzi ukafanyika kwamba makao makuu yajengwe hapa Nairobi? Wanafaa waangalie kihaki kabisa, na watuonyeshe ilikuwa vipi Nairobi ikachaguliwa kama pahali patakapotengezwa makao hayo makuu.

Bw. Spika wa Muda, sitaki kusema mengi, lakini naunga mkono hii taarifa iliyoletwa na Sen. Faki. Wale waliopanga njama ya kupendekeza makao haya yawe Nairobi, basi wajue kwamba ukweli utajulikana.

Asante sana, Bw. Spika wa Muda.

*[The Temporary Speaker (Sen. (Dr.) Lelegwe) left the Chair]*

*[The Deputy Speaker (Sen. (Prof.) Kindiki) in the Chair]*

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindik): Order, Senators! I will allow two more Senators.

Proceed, Sen. (Dr.) Ali.

**Sen. (Dr.) Ali:** Thank you, Mr. Deputy Speaker, Sir. *Watu wananiambia niongee Kiswahili, lakini*---

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Order, Sen. (Dr.) Ali! Umeambiwa na watu wapi?

**Sen. (Dr.) Ali:** Maseneta wenzangu wanasema niongee Kiswahili. Nataka kuwaambia kuwa naelewa Kiswahili sanifu kabisa.

*(Laughter)*

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Proceed, Sen. (Dr.) Ali.

**Sen. (Dr.) Ali:** Bw. Naibu Spika, natakubaliana na Sen. Faki kwa sababu taarifa aliyoileta hapa ni wa maana kabisa. Ile tabu tuko nayo ni kuwa katika nchi hii, wakitaka kufanya kitu chochote, mahali pa kwanza wanapofikiria ni Nairobi. Nairobi imekuwa jangwa la ukuta. Kuna dunia nyingine iliyo na nafasi ya kutosha na wako na haki ya kuwa na makao makuu ya mradi wowote. Kama kila kitu kitafanywa hapa Nairobi, wale watu wengine wataenda wapi? Ni maajabu! Kwa mfano, wanasema mambo ya uvuvi yaletwe hapa Nairobi. Mambo ya wanyama wa pori yanataka kuletwa Nairobi. Kila kitu wakifikiria ni Nairobi.Hiyo haifai.

Badala ya watu kusukumana hapa na pale, nafikiri huko kwetu, iwapo maji ya Tana River yatapelekwa upande wa Wajir, basi tutakuwa na ziwa kubwa sana. Pengine hata hili jangwa la ukuta lipelekwe huko Wajir badala ya kuletwa Nairobi.

Bw. Naibu Spika, langu ni kumsaidia Sen. Faki, na kusema ukweli wa mambo ili Kamati husika iangalie maneno haya kwa makini. Tunataka Kamati hii imuite Waziri na wote wanaohusika ili kufafanua zaidi juu ya swala hili. Kama ni mambo ya kula na mengineyo, hata Mombasa na Kilifi mambo haya yanaweza kufanyika.

Bw. Naibu Spika, naunga mkono taarifa hii.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Sen. Mwaura, be brief.

**Sen. Mwaura**: Asante sana, Bw. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii kuchangia taarifa ambayo imeletwa na Sen. Faki. Ni muhimu kuhakikisha kwamba katika mwito wa ugatuzi tunagatua taasisi za kitaifa ambazo zinajiuzisha hususan na maswala ya kilimo. Ni jambo la kushangaza kwamba Nairobi hakuna samaki wengi. Iweje makao makuu ya hii taasisi yawe Nairobi?

Tuendelee kugatua shughuli nyingi ili kuwe na uwakilishaji wa Serikali Kuu katika Kaunti ya Nairobi lakini tuanze kujenga miji mingine ili iweze kustawisha biashara na Wakenya waweze kwenda kule kwa sababu hapa Nairobi tunamsongamano mkubwa ambao unazuia uendeshaji wa shughuli za kiuchumi.

Bw. Naibu Spika, naunga mkono.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Thank you, for being brief. If you maintain that pace, I will allow a few more.

Proceed, Sen. Madzayo.

*(Sen. Madzayo spoke off-record)*

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Give Sen. Madzayo the microphone.

**Sen. Madzayo**: Asante, Bw. Naibu Spika. Hapo awali, ulitueleza kwamba kuna watoto kutoka Kajiado County ambao mpaka sasa wako pale juu.

Nina kuunga mkono kwa kuwakaribisha kwa dhati. Ninawapa kongole walimu na watoto ambao wako katika madarasa ya chini kwa kuja katika Bunge la Seneti ili wasikie, watafakari na waoene Maseneta pamoja na Spika na vile tunafanya mambo yetu. Wao ni viongozi wa siku za usoni.

Ninawapa changamoto ya kwamba hakuna lisilowezekana katika ndoto zao. Kama wanataka kuwa Maseneta siku moja, hiyo ndoto inawezekana. Kwa hivyo, wafanye bidii.

Nimeketi katikati ya Maseneta wanaotoka katika kaunti za uchungaji. Shule hii ni moja wa shule nyingi inatoka katika sehemu za uchungaji. Upade wa kushoto niko na dadangu Sen. Pareno na upande wa kulia niko na kakangu, Sen. Olekina.

**Sen. Sakaja**: On a point of order, Mr. Deputy Speaker, Sir.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): What is it, Sen. Sakaja?

**Sen. Sakaja**: Bw. Naibu Spika, imekuwa desturi kwamba tunapozungumza Kiswahili tunahimizana tuzungumze Kiswahili sanifu. Ndugu yangu ambaye siwezikumfunza Kiswahili hata kidogo, Seneta wa Kilifi, amesema ya kwamba wezake, Sen. Olekina na Sen. Pareno wanatoka kaunti za uchungaji.

**Sen. Madzayo**: Nimesema, wafugaji.

**Sen. Sakaja:** Amesema tena kwa mara ya pili 'wachungaji'. Ukiangalia Nakala ya Bunge, utaona ya kwamba amesema 'wachungaji'. Wachungaji ninavyowajua ni wale makasisi na wanaohubiri. Ni wachungaji au wafugaji? Lakini sijasema kaunti hizo hazina wachungaji.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Order! Proceed, Sen. Madzayo.

**Sen. Madzayo**: Asante, Bw. Naibu Spika. Kuna tofauti ya watumishi wa Mungu na wafugaji au wachungaji. Nikizingatia mambo ya---

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): You have not answered Sen. Sakaja's concerns.

**Sen. Madzayo:** Bw. Naibu Spika, amesema kwamba nimetumia neno 'wachungaji' ambalo hata ndani ya Bibilia linamaanisha mtu anayetafuta kondoo aliyepotea na kumleta nyumbani.

Nimesema kwamba hawa ndugu zangu wanaishi katika sehemu ambapo wanafuga mifugo kama vile ndugu yangu Sen. (Dr.) Ali anafuga ngamia, hawa wanafuga ng'ombe ambao wanatupatia maziwa na bidhaa zingine. Ndio maana nilisema nimeketi katikati ya dadangu na kakangu ambao ni Maseneta wa nguvu kutoka maeneo ya Kajiado na Narok.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Conclude, Sen. Madzayo.

**Sen. Madzayo:** Bw. Naibu Spika, hawa hawakupata nafasi hii kwa urahisi. Walifanya bidii wakiwa watoto kama nyinyi katika sehemu za ufugaji. Kwa hivyo, nyinyi mnaweza kuwa kama wao.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Sen. Sakaja, 'wafugaji' are keepers of livestock. Wachungaji are herdsmen who go out there to take care of animals. 'Wafugaji' are people whose livelihood is derived from keeping livestock.

Proceed, Sen. Mutula Kilonzo Jnr. you are normally brief. I am sure that you will do it in a minute. I hope that it is not about the students because we have already welcomed them.

**Sen. Mutula Kilonzo Jnr.:** Asante, Bw. Naibu Spika. Ninataka kuzungumza kwa kifupi kuhusu taarifa ambayo imewasilishwa na Sen. Faki. Kitu ambacho amesahau kukiweka katika taarifa yake ni kama Bw. Mbotela angeuliza, je, ni ungwana kweli kwamba makao ambayo yatazingatia uvuvi yajengwe eneo la South B, mahali ambapo Seneta wa Nairobi anamiliki?

Sijaona jambo hili katika taarifa ambayo amewasilisha kama Serikali Kuu iliwaita Wakenya wanaotoka eneo la Pwani ili wapate mawaidha. Lakini, jambo hili lazima lizungumziwe.

Hatushangai kwa sababu jambo ambalo linafanya Wachina kuleta samaki Kenya ndilo swala unaloliona kwamba wavuvi wanaotoka katika sehemu za Nyanza, Mombasa na Pwani wametupiliwa mbali na kuwachwa nyuma kimaendeleo. Vitu ambavyo vinazungumziwa na wafadhili ni jambo ambalo linaweza kuleta ajira.

Ndugu yangu na kaka yangu ambaye Seneta wa Bugoma anamwita *distinguished nephew*, Sen. Sakaja amepitisha Mswada ambao ungepatia vijana kazi. Vijana wengi wa Mombasa wangepata kazi kama *headquarters* zingejengwa katika eneo la Pwani. Kwa hivyo, lazima jambo hili liangaliwe kwa kimakini kwa sababu linaweza kuleta mapato kwa Serikali ya Kaunti ya Mombasa na Serikali Kuu. Jambo hili lifutiliwe mbali.

Wakati mwingine, ukiangalia mambo yanayofanywa na Serikali ya Jubilee, utafikiria kuna mazingaumbwe Kenya.

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Say what has not been said by other Senators.

Proceed, Sen. Zawadi. You have one minute.

**Sen. Zawadi:** Asante, Bw. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii niweze kuzungumza kuhusu taarifa ambao iko mbele yetu. Namshukuru Mhe. Sen. Faki.

*(Sen. Mutula Kilonzo Jnr. consulted loudly)*

**The Deputy Speaker** (Sen. (Prof.) Kindiki): Order, Sen. Mutula Kilonzo Jnr.! Are you laughing at yourself or at Jubilee?

Proceed, Sen. Zawadi.

**Sen. Zawadi**: Asante, Bw. Naibu Spika. Nakubaliana na wezangu ambao wamezungumza mbeleni kwamba yale yanataka kufanyika ni unyanyapaa wa hali ya juu. Sisi watu wa Pwani, hasa Kilifi, Mombasa na Kwale ni Wakenya kama Wakenya wengine. Kwa hivyo, kama peas zimekuja kama zimetulenga, wachazitufikie.

Kama kitu ni kizuri, kinakuja Nairobi. Mtu wa Kilifi akitaka msaada, atatoka Mombasa, Kilifi au Tana River mpaka Nairobi. Hiyo si ungwana. Maana ya ugatuzi ni nini ikiwa watu watatoka kule mashinani na kuja Nairobi? Watu wa chini wanafaa kufaidika na kuinuka kiuchumi. Kama ni nyumba za kupangisha, wale watakua maofisini wataenda kupangisha nyumba hizo na biashara itasongea.

Ninaungana na wenzangu kwamba si haki zile ofisi zije Nairobi kwa sababu bahari iko Pwani. Ninauhakika watu kama wale wangepewe nafasi, wangehamisha bahari lakini Mwenyezi Mungu alipanga iwe kule. Wacha watu wa Pwani wafaidike na wale

matunda yao. Mwenyezi Mungu aliwaumba na kuwaweka kule, kwa hivyo, wacha wale matunda yao.

**Sen. Olekina:** Bw. Naibu Spika, shukrani kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa hii ya mipango ya Serikali Kuu kujenga kwa niaba ya kaunti tano. Sisi sote tunajua ya kwamba, kaunti hizi ni kaunti za uvuvi. Huu ni utendakazi ambao umegatuliwa.

Katika serikali ya ugatuzi, ni lazima sisi kama Seneti ya Kenya tujaribu kuhakikisha ya kwamba, majukumu ambayo yamegatuliwa yafaidi wale watu walio katika kaunti.

Tujenga makao haya hapa Nairobi ni madharau na upotuvu wa nidhamu na heshima kwa watu wa maeneo ya pwani. Mimi kama Seneta wa Kaunti ya Narok ninalipinga jambo hilo kabisa. Wakianza kuleta kila jukumu hapa Nairobi, kesho watasema kwamba ni lazima wajenge jumba kuu linaloshughulikia mambo kuhusu uuzaji na ununuzi wa nyama na ngano yote ambyo inatoka Narok hapa jijini.

Tukikubali hayo yatendeke, tutakua tunafungua njia ya kaunti zetu zote kunyanyaswa na kufanywa kuwa maskini. Jambo hili ni dhuluma---

**The Deputy Speaker (**Sen. (Prof.) Kindiki)**:** You are making observations. We are not debating. It is a Statement. Just make observations.

**Sen. Olekina:** Bw. Naibu Spika, kitendo hicho ni kama kutoa nyama kwa mdomo. Sisi kama Maseneta ambao tumekuja katika Bunge hili ili tuweze kuwa kitu kimoja, tunaipinga.

Ningependa kwanza kuomba kwamba makao ya Waziri wa Kilimo, ufugaji na uvuvi yanastahili kuwa katika maeneo ya pwani. Hii ni kwa sababu jimbo la pwani linaweza kulisha Kenya yote kwa issue ya *samaki*.

Shukrani.